MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

MSAMAHA WA ADHABU KWA MAGARI YALIYOKIUKA SHERIA NA TARATIBU ZA FORODHA

Dar es Salaam, 2 Oktoba, 2026:

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuufahamisha Umma, hususan wamiliki na watumiaji wa magari yaliyokiuka Sheria na Taratibu za Forodha, kuwa imetoa msamaha maalum wa adhabu kwa lengo la kutoa fursa ya kujitokeza kwa hiari, kurekebisha kasoro za kiforodha na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria.

Kupitia utaratibu huu, watu wote wanaohusika wanahimizwa kujitokeza kwa hiari katika Ofisi za TRA zilizo karibu nao ili kurekebisha hadhi ya kiforodha ya magari yao kabla au ifikapo tarehe 31 Desemba 2026.

Msamaha huu unahusu magari yenye makosa yafuatayo ya kiforodha:

1. **Matumizi mabaya ya utaratibu wa Uingizaji wa Muda (Temporary Importation Regime)**;
2. **Upotoshaji wa mwaka wa kutengenezwa au modeli ya gari** kwa nia ya kupunguza ushuru na kodi stahiki;
3. **Kubadilisha, kuharibu au kuingilia utambulisho wa chassis/VIN;**
4. **Matumizi yasiyo sahihi ya Kanuni za Uasili wa Bidhaa za SADC (SADC Rules of Origin);**
5. **Matumizi mabaya ya misamaha ya kodi;**
6. **Kuchepusha mizigo ya transit pamoja na udanganyifu wa taarifa za kutoka nchini;** na
7. **Uainishaji usio sahihi (misclassification) pamoja na ubadilishaji usioidhinishwa wa muundo, maelezo au matumizi ya bidhaa.**

Wamiliki au watumiaji wa magari yanayohusika na makosa hayo wanahimizwa kutumia fursa hii kwa kujitokeza kwa hiari TRA, kutoa taarifa sahihi kuhusu ukiukwaji uliofanyika na kulipa ushuru na kodi stahiki, kwa kuzingatia masharti yatakayotumika katika utekelezaji wa msamaha huu.
Msamaha huu utatumika hadi tarehe **31 Desemba, 2026**. Baada ya muda huo, TRA itachukua hatua stahiki za kiutekelezaji kwa magari yatakayobainika kukiuka Sheria na Taratibu za Forodha, kwa mujibu wa sheria.

Hivyo, Umma unahimizwa kutumia fursa hii kwa wakati ili kurekebisha hadhi ya kiforodha ya magari husika na kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria na Taratibu za Forodha.

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

Imetolewa na;

Yusuph Juma Mwenda
KAMISHNA MKUU